Imeandaliwa na:
Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia
Wanawake na Makundi Maalum
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya
S.L.P 573, 404080 DODOMA
Simu Na. +255 (026) 2963341/2963346
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz,
Nukushi: 255 (026) 2963348

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# MWONGOZO WA UTOAJI WA MIKOPO YENYE MASHARTI NAFUU KWA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO KUPITIA TAASISI ZA FEDHA




SEPTEMBA, 2024

DODOMA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# MWONGOZO WA UTOAJI WA MIKOPO YENYE MASHARTI NAFUU KWA WAFANYABIASHARA NDOGONDOGO KUPITIA TAASISI ZA FEDHA

**SEPTEMBA, 2024** **DODOMA**

YALIYOMO


TAFSIRI YA MANENO .................................................................. iv

DIBAJI ....................................................................................... v

SURA YA KWANZA ..................................................................... 1

UTANGULIZI ............................................................................... 1

1.1 Dhana na Hali Halisi ya Wafanyabiashara Ndogondogo Nchini .. 1

1.2 Umuhimu wa Mwongozo ........................................................ 1

1.3 Walengwa wa Mwongozo ....................................................... 2

1.4 Malengo ya Mwongozo .......................................................... 2

1.5 Matokeo Tarajiwa ................................................................. 3

SURA YA PILI ............................................................................. 4

VYANZO VYA FEDHA NA URATIBU WA MIKOPO ........................ 4

2.1 Vyanzo vya Fedha za Mikopo ................................................ 4

2.2 Utaratibu wa Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo .......................... 4

2.2.1 Utaratibu wa Utoaji wa Mikopo .............................................. 4

2.2.2 Utaratibu wa Urejeshaji Mikopo ............................................. 5

SURA YA TATU .......................................................................... 6

MASHARTI YA MKOPO ............................................................... 6

3.1 Walengwa wa Mkopo ........................................................... 6

3.2 Sifa za Mwombaji wa Mkopo ................................................. 6

3.3 Muda wa Mkopo na Riba ....................................................... 7

SURA YA NNE ............................................................................ 8

MFUMO WA KITAASISI ............................................................... 8

4.1 Utangulizi ............................................................................ 8

4.1.1 Wizara yenye Dhamana na Makundi Maalum .......................... 8

4.1.2 Wizara ya Fedha .......................................................................... 9

4.1.3 Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) ........................................................................................ 9

4.1.4 Taasisi ya Fedha Inayotoa Mikopo ....................................... 10

4.1.5 Sekretarieti za Mikoa ............................................................ 10

4.1.6 Mamlaka za Serikali za Mitaa .............................................. 11

4.1.7 Viongozi wa Wafanyabiashara Ndogondogo .......................... 11

4.1.8 Wafanyabiashara Ndogondogo ............................................. 12

SURA YA TANO ........................................................................... 13

UFUATILIAJI, TATHMINI NA UKAGUZI ....................................... 13

5.1 Ufuatiliaji na Tathmini ........................................................... 13

5.2 Utunzaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Utoaji Mikopo ............ 14

5.3 Mapitio ya Mwongozo ............................................................ 14

5.4 Ukaguzi wa Fedha za Mikopo ................................................ 15

5.5 Uwajibikaji Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Utoaji Mikopo ........................................................................................... 15

SURA YA SITA ............................................................................. 16

HITIMISHO .................................................................................. 16

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **NIDA** | National Identification Authority. |
| **OR – TAMISEMI** | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. |
| **SIDO** | Small Industries Development Organization. |
| **VETA** | Vocational Education and Training Authority. |
| **WBN-MIS** | WafanyaBiashara Ndogondogo - Management Information System. |

# TAFSIRI YA MANENO

**Dawati maalum la uratibu wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo:** Ni dawati ambalo litaanzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kurahisisha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za kila siku za wafanyabiashara ndogondogo na litakuwa chini ya Idara ya Maendeleo ya Jamii.

**Mfanyabiashara Ndogondogo kwa mujibu wa Mwongozo huu:** Ni mjasiriamali aliye kwenye sekta isiyo rasmi, anayeuza bidhaa au kutoa huduma inayotambuliwa na mauzo ghafi yake hayazidi shilingi 4,000,000/= kwa mwaka. Wafanyabiashara hao ni wale walio kwenye sekta za kilimo, viwanda vidogovidogo, uchimbaji madini, usafirishaji, utalii, ujenzi, uvuvi na ufugaji.

**Sekta Isiyo Rasmi:** Ni Sekta ambayo inabeba idadi kubwa ya watu wanaojipatia kipato chao cha kila siku kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi. Baadhi ya watu katika Sekta hii hawana sehemu rasmi ya kufanyia biashara, hawana leseni za biashara, hawana vitambulisho vya biashara na pia hawalipi kodi ya mapato.

# DIBAJI

Shughuli za kiuchumi kwa wafanyabiashara ndogondogo, wakiwemo machinga, waendesha pikipiki, bajaji, guta, mama/baba lishe na watoa huduma ni muhimu katika kuinua kipato na ukuzaji wa ajira kwa vijana na wanawake katika sekta isiyo rasmi kwa nchi nyingi zinazoendelea. Ili kuinua na kurasimisha sekta hiyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti ya kuinua sekta hiyo kiuchumi. Baadhi ya hatua na afua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo; uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi kwa wafanyabiashara hao; utoaji wa elimu ya ujasiriamali pamoja na elimu ya fedha.

Pamoja na jitihada hizo, bado wafanyabiashara hao wanakabiliwa na changamoto zinazokwamisha maendeleo yao ikiwemo:- ukosefu wa dhamana ili kuwawezesha kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za Fedha; wengi wanaofanya kazi kwenye sekta isiyo rasmi kwa kiasi kikubwa shughuli zao za kiuchumi hazionekani katika Pato la Taifa na baadhi hawalipi kodi; miradi mingi ya kusaidia wafanyabiashara ndogondogo haifanyi vizuri kwa kuwa baadhi hawarejeshi mikopo na hivyo kusababisha kupungua kwa mtaji; na baadhi ya wafanyabiashara ndogondogo wanashindwa kupata mikopo na kurejesha kwa kuwa hawana vitambulisho vinavyowatambulisha kwenye Taasisi za Fedha zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali.

Kutokana na changamoto hizo, Serikali imeandaa Mwongozo huu kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Taasisi za Fedha zilizokasimiwa kutoa mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo waliotambuliwa, kusajiliwa na kupatiwa vitambulisho vya kidijitali. Wafanyabiashara hao ni wale wanaojishughulisha na biashara katika sekta za kilimo, viwanda vidogovidogo, uchimbaji madini, usafirishaji, utalii, ujenzi, uvuvi, ufugaji na utoaji huduma. Utoaji wa mikopo yenye masharti

nafuu unatarajiwa kuchochea ukuaji wa mitaji kwa wafanyabiashara ndogondogo.

Kwa muktadha huo, utekelezaji wa Mwongozo huu utasaidia kuweka mifumo endelevu ya utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara hao kwa lengo la kuimarisha shughuli zao za kiuchumi ili kuwawezesha kukua na kuwa wafanyabiashara wa Kati na Wakubwa watakaoleta tija katika maendeleo ya nchi. Vilevile, kwa kufanya hivyo, Serikali itarahisisha urasimishaji wa wafanyabiashara ndogondogo katika sekta isiyo rasmi na kuwezesha wahusika kunufaika na fursa za kiuchumi kupitia taasisi za fedha ili kukuza kipato chao.

.....................................

Dkt. Seif A. Shekalaghe

**KATIBU MKUU**

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Dhana na Hali Halisi ya Wafanyabiashara Ndogondogo Nchini

Wafanyabiashara ndogondogo wanaoratibiwa na Wizara yenye dhamana wamegawanyika katika makundi mbalimbali kutokana na namna ambavyo wanafanya biashara zao. Makundi hayo ni pamoja na wachuuzi wa bidhaa; wanaopanga bidhaa zao chini au mezani; wale wanaotembeza bidhaa kwa mikokoteni, baiskeli na mikononi; waendesha bodaboda na bajaji; mama na baba lishe; wasusi; na makundi mengine kwa kadri yanavyoendelea kutambuliwa.

Kwa mujibu wa matokeo ya awali ya Sensa ya Watu na Makazi (2022), makundi hayo yanajumla ya wafanyabiashara ndogondogo 1,175,617 (Me 496,496; Ke 679,121) Tanzania Bara. Kwa sehemu kubwa, biashara za wafanyabiashara hao hufanyika katika maeneo yasiyo rasmi yenye mikusanyiko mikubwa ya watu, au kwa kutembeza bidhaa na kuwafuata wateja walipo kwenye maeneo yao.

Wafanyabiashara hao wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika shughuli zao za kila siku ikiwa ni pamoja na ugumu wa kupata mikopo kutokana na kushindwa kukidhi vigezo na masharti yanayowekwa na taasisi za fedha.

## 1.2 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo unatokana na nia ya Serikali kupitia Wizara yenye dhamana na Makundi Maalum kuamua kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa wafanyabiashara ndogondogo. Mwongozo huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Viwanda VidogoVidogo (2003), Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2017, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya Mwaka 2004.

Mwongozo huu unawezesha kufikiwa kwa lengo la Mwongozo wa Uratibu na Usajili wa Wafanyabiashara Ndogondogo wa Mwaka 2024. Pia ni nyenzo muhimu ya kuratibu, kusimamia na kufuatilia utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara kupitia Taasisi husika kwa ushirikiano na Serikali katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## 1.3 Walengwa wa Mwongozo

Miongoni mwa wadau watakaotumia Mwongozo huu ni watendaji wa Serikali katika ngazi zote, Wafanyabiashara ndogondogo, Wadau wa Maendeleo na Sekta Binafsi katika jitihada za kuwezesha Wafanyabiashara Ndogondogo Nchini.

## 1.4 Malengo ya Mwongozo

Kuweka mfumo wa uratibu na usimamizi na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini ili kuinua kipato chao na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Malengo Mahsusi ya Mwongozo ni:-

i) Kuwezesha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini kupitia Taasisi husika kwa ajili ya kukuza na kupanua shughuli zao za kiuchumi ili kuongeza fursa za ajira zinazochochea ukuaji wa uchumi jumuishi;

ii) Kuainisha majukumu na wajibu wa wadau wakati wa utekelezaji wa shughuli ya utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo katika kila ngazi; na

iii) Kuweka mfumo wa upatikanaji, utunzaji na utoaji wa taarifa ya maendeleo ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini.

## 1.5 Matokeo Tarajiwa

Matokeo yanayotarajiwa baada ya kutekelezwa kwa Mwongozo huu ni:-

i) Kuongezeka kwa fursa ya upatikanaji wa mitaji ya kupanua shughuli za kiuchumi miongoni mwa wafanyabiashara ndogondogo na ukuaji wa fursa za ajira;

ii) Kuimarika kwa mifumo ya uratibu, usimamizi na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;

iii) Kuboreshwa kwa mazingira ya biashara ndogondogo na urasimishwaji wa sekta isiyo rasmi nchini;

iv) Kuboreshwa kwa ujuzi wa usimamizi wa fedha miongoni mwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;

v) Kuongezeka kwa kipato na kupungua kwa umaskini miongoni mwa wafanyabiashara ndogondogo nchini; na

vi) Kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo kuwa wafanyabiashara wa kati na wakubwa na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

# SURA YA PILI

# VYANZO VYA FEDHA NA URATIBU WA MIKOPO

## 2.1 Vyanzo vya Fedha za Mikopo

Chanzo kikuu cha fedha za mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini itakuwa ni bajeti ya Serikali pamoja na marejesho ya mikopo hiyo kutoka kwa wafanyabiashara ndogondogo. Washirika wa Maendeleo na Wafadhili wataweza kuchangia Mpango huo kwa kadri utakavyokuwa unatekelezwa ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika eneo hilo la kuwezesha makundi hayo kiuchumi.

## 2.2 Utaratibu wa Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo

Utaratibu wa utoaji na urejeshaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini utafanyika kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya Taasisi ya Fedha husika iliyoingia makubaliano na Serikali.

### 2.2.1 Utaratibu wa Utoaji wa Mikopo

Fedha za mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo zitatolewa na Serikali pamoja na wadau wengine ambapo Wizara ya Fedha itapeleka fedha hizo kwenye Taasisi ya Fedha husika kwa kuzingatia utaratibu utakaokuwa umekubaliwa baada ya Taasisi ya Fedha husika kuingia mkataba na Serikali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini.

Hatua zifuatazo zitazingatiwa:-

i) Mwombaji atajaza fomu ya maombi ya mkopo inayopatikana katika Taasisi za Fedha zikiwemo Benki zilizoingia mkataba na Wizara yenye dhamana;

ii) Maombi yote yatahakikiwa na kuchambuliwa kwa kina na Taasisi husika;

iii) Waombaji walioomba mkopo watajulishwa juu ya maendeleo ya maombi yao na Taasisi husika;

iv) Waombaji waliokidhi vigezo wataingiziwa fedha zao kwenye akaunti au kupatiwa vifaa kulingana na aina ya mkopo walioomba; na

v) Muda wa kushughulikia mkopo baada ya kuwasilisha nyaraka zote utazingatia taratibu za Taasisi ya Fedha husika.

### 2.2.2 Utaratibu wa Urejeshaji Mikopo

Mikopo yote itakayotolewa kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini itarejeshwa na wafanyabiashara hao katika Taasisi ya Fedha husika. Urejeshaji huo utazingatia taratibu zifuatazo:-

i) Marejesho yatafanyika kulingana na makubaliano ya Mkataba wa mkopo baina ya Mkopaji na Taasisi ya Fedha husika; na

ii) Taasisi ya Fedha husika itaandaa taarifa za utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa kila robo mwaka wa fedha na kuziwasilisha katika Wizara yenye dhamana.

## SURA YA TATU

## MASHARTI YA MKOPO

### 3.1 Walengwa wa Mkopo

Wanufaika wa Mkopo wenye masharti nafuu kupitia Taasisi za Fedha ni wafanyabiashara ndogondogo kama ilivyotafsiriwa kwenye Mwongozo huu. Wafanyabiashara hao ni pamoja na:-

i) Machinga;

ii) Waendesha pikipiki (bodaboda) za miguu miwili, miguu mitatu na guta;

iii) Mama na baba lishe; na

iv) Makundi mengine ya wafanyabiashara hao kwa kadri yatakavyokuwa yanatambuliwa na Mamlaka na kusajiliwa katika mfumo wa wafanyabiashara ndogondogo.

### 3.2 Sifa za Mwombaji wa Mkopo

Sifa zinazohitajika wakati wa kuomba mkopo:-

i) Mwombaji awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea;

ii) Mwombaji awe na kitambulisho cha Mfanyabiashara Ndogondogo kinachotolewa kupitia mfumo wa utambuzi na usajili (WBN-MIS) unaosimamiwa na Wizara yenye dhamana;

iii) Mwombaji awe na biashara inayotambuliwa na Mamlaka katika eneo husika;

iv) Mwombaji awe tayari kufungua akaunti katika Taasisi ya Fedha husika inayotoa mikopo hiyo;

v) Mwombaji awe tayari kukidhi vigezo kutoka kwenye Taasisi ya Fedha husika inayotoa mikopo hiyo;

vi) Mwombaji awe na nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Namba ya NIDA; na

vii) Mwombaji awe kwenye eneo linalotambuliwa na Mamlaka kwa ajili ya kufanyia biashara; mfano soko.

### 3.3 Muda wa Mkopo na Riba

Muda wa mkopo na riba itakayotozwa kwa walengwa ni kama ifuatayo:

i) Muda wa mkopo utakuwa ni kuanzia miezi mitatu (3) hadi miezi 24 na utategemea aina ya biashara Mwombaji ameombea mkopo;

ii) Mkopo utatozwa riba ya asilimia saba (7%), ambapo asilimia tano (5%) itatumiwa na Taasisi husika kwa ajili ya shughuli za utawala na usimamizi; asilimia moja (1%) itatumiwa na Serikali kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo katika ngazi mbalimbali; na asilimia moja (1%) itakuwa kwa ajili ya kurejeshwa kwenye mfuko ili fedha iwe endelevu; na

iii) Mkopo utatozwa bima dhidi ya kifo na ulemavu wa kudumu kwa mkopaji.

# SURA YA NNE

# MFUMO WA KITAASISI

## 4.1 Utangulizi

Majukumu ya Serikali kwa kushirikiana na wadau katika utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji Mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini yatakuwa kama ifuatavyo:-

### 4.1.1 Wizara yenye Dhamana na Makundi Maalum

i) Kuandaa na kufanya mapitio ya miongozo, mikataba, mikakati na programu za kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo nchini;

ii) Kuratibu utoaji wa elimu ya ujasiriamali kabla na baada ya kutoa mikopo kwa walengwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Fedha husika husika pamoja na Maafisa wa Serikali katika Halmashauri za Wilaya;

iii) Kuratibu uandaaji wa taarifa ya kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka ya utekelezaji wa mradi wa utoaji mikopo yenye masharti nafuu;

iv) Kuimarisha mfumo wa utambuzi na usajili wa wafanyabiashara ndogondogo (WBN - MIS) ili kuwa na taarifa na takwimu sahihi na kwa wakati;

v) Kujenga uwezo wa Waratibu wa shughuli za Makundi Maalum ngazi ya Mikoa na Halmashauri ili kuboresha utendaji wao;

vi) Kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;

vii) Kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kutoa huduma ya mikopo kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;

viii) Kupanga na kuratibu vikao vya kila robo, nusu na mwaka vya Wizara za Kisekta zinazohusika na shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara ndogondogo nchini; na

ix) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika ufuatiliaji wa wakopaji kupitia Taasisi ya Fedha husika katika Halmashauri mbalimbali nchini.

### 4.1.2 Wizara ya Fedha

i) Kuhakikisha kuwa Wizara za Kisekta zinatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuimarisha biashara za wafanyabiashara ndogondogo nchini;

ii) Kuhakikisha kuwa inatoa fedha kwa Wizara yenye dhamana na Makundi Maalum kwa ajili ya kuratibu shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara ndogondogo nchini;

iii) Kuhakikisha kuwa rasilimali fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za kuimarisha biashara ndogondogo zinatolewa kwa wakati;

iv) Kuratibu Taasisi za Fedha ili zishirikiane na Serikali katika kuwezesha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara ndogondogo nchini hasa katika kipengele cha mikopo yenye riba nafuu; na

v) Kuhakikisha kuwa Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali unaotolewa kila mwaka unajumuisha masuala ya wafanyabiashara ndogondogo.

### 4.1.3 Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI)

i) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatenga na kuendeleza maeneo pamoja na kuweka miundombinu stahiki na rafiki kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara ndogondogo nchini;

ii) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasajili wafanyabiashara ndogondogo kwenye mfumo ili wapate vitambulisho vya kidijitali; na

iii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za kuendeleza wafanyabiashara ndogondogo kiuchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 4.1.4 Taasisi ya Fedha Inayotoa Mikopo

i) Kuhakikisha fomu za maombi ya mikopo zinapatikana kwa wakati kwenye matawi yake nchi nzima;

ii) Kusimamia utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa marejesho kwa kuzingatia taratibu za Taasisi husika;

iii) Kutoa elimu ya fedha kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;

iv) Kuelimisha wafanyabiashara ndogondogo kuhusu uwepo wa mikopo na huduma mbalimbali za kifedha;

v) Kuhakikisha kuwa wakopaji wote wanarejesha mikopo yao kwa wakati ili kuwezesha wengine kukopa; na

vi) Kuandaa taarifa za utoaji mikopo kwa mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka na kuziwasilisha Wizara yenye dhamana na Makundi Maalum.

### 4.1.5 Sekretarieti za Mikoa

i) Kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara ndogondogo katika Halmashauri zote ndani ya Mkoa;

ii) Kuratibu na kusimamia utambuzi, usajili na ugawaji vitambulisho vya kidijitali kwa wafanyabiashara ndogondogo;

iii) Kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini kupitia Taasisi husika; na

iv) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya uratibu, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi za wafanyabiashara ndogondogo kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka na kuwasilisha OR - TAMISEMI.

### 4.1.6 Mamlaka za Serikali za Mitaa

i) Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;

ii) Kuhakikisha mfanyabiashara ndogondogo mwenye sifa anatambuliwa, anasajiliwa na kupatiwa kitambulisho cha kidijitali;

iii) Kuhakikisha wafanyabiashara ndogondogo wanafanya shughuli zao za kiuchumi katika masoko au maeneo rasmi yaliyotengwa kwa ajili yao;

iv) Kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu ya masuala ya fedha na mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo;

v) Kuhamasisha wafanyabiashara ndogondogo kuhusu uwepo wa fursa za kiuchumi kwenye taasisi wezeshi ikiwemo Benki, SIDO na VETA;

vi) Kutambua, kusajili na kusambaza vitambulisho kwa wafanyabiashara ndogondogo ili waweze kunufaika na mikopo yenye masharti nafuu kupitia Taasisi ya Fedha; na

vii) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za uratibu wa wafanyabiashara ndogondogo kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka na kuziwasilisha katika ngazi ya Mikoa.ben

### 4.1.7 Viongozi wa Wafanyabiashara Ndogondogo

i) Kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara ndogondogo anatambuliwa na kusajiliwa kwenye mfumo wa WBN-MIS;

ii) Kushirikiana na Serikali na wadau kuratibu mafunzo kwa wafanyabiashara ndogondogo kwa ajili ya kujiongezea ujuzi na maarifa kuhusiana na masuala ya fedha na biashara;

iii) Kutoa taarifa sahihi za wafanyabiashara ndogondogo kwa Maafisa wa Taasisi ya Fedha na Mamlaka zingine pindi zinapohitajika; na

iv) Kuwa Mawakala wa kulinda na kutunza amani na utulivu kwenye maeneo yao ya kufanyia biashara.

### 4.1.8 Wafanyabiashara Ndogondogo

i) Kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi na usajili wa wafanyabiashara ndogondogo (WBN-MIS);

ii) Kushiriki mafunzo kwa ajili ya kujiongezea ujuzi na maarifa kuhusiana na masuala ya fedha na biashara;

iii) Kutoa taarifa sahihi za biashara yake kwa Maafisa wa Taasisi ya Fedha na Mamlaka zingine pindi zinapohitajika; na

iv) Kuhakikisha kuwa mkopo unarejeshwa kwa wakati ili kuruhusu wengine kukopa.

# SURA YA TANO

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UKAGUZI

## 5.1 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji ni hatua madhubuti inayohusisha kukusanya, kuchambua na kutumia taarifa za utekelezaji katika kufanya maamuzi ili kufikia lengo la mradi lililokusudiwa. Hivyo, ufuatiliaji unasaidia kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi ikiwemo mchakato wa utekelezaji na matokeo yaliyokusudiwa.

Tathmini ni mchakato wa kupima na kupata mrejesho wenye malengo ya kuangalia utaratibu, utekelezaji na matokeo ya mradi uliokusudiwa. Tathmini inalenga kuchunguza na kupima utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia vigezo maalumu vya ufanisi, umuhimu, uendelevu, kufungamanisha na afua nyingine na matokeo ya muda mrefu.

Hivyo, ufuatiliaji na tathmini utafanyika katika ngazi zote zinazohusika na utoaji wa mikopo hiyo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini. Kwa msingi huo, ufuatiliaji utafanyika na taarifa zitaandaliwa kila robo mwaka kwa ajili ya kubaini changamoto zinazohitaji kurekebishwa mapema wakati wa utekelezaji katika kila ngazi.

Tathmini ya utoaji wa Mikopo itafanyika kuona kama:-

i. Wafanyabiashara ndogondogo ambao ndiyo walengwa wa mkopo huo wameweza kubadilisha hali ya uchumi wao baada ya kupata mkopo husika. Hivyo, tathmini itafanywa na Maafisa wa Serikali kwa kushirikiana na Maafisa wa Taasisi ya Fedha husika katika Halmashauri mbalimbali nchini; na

ii. Tathmini nyingine itahusu mradi huo wa utoaji mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo kwa lengo la kupanua wigo, ubora na ufanisi wa mradi pamoja na kuendeleza huduma zinazotolewa kupitia mradi huo. Tathmini hiyo itajumuisha wadau wengine wanaovutiwa na urasimishwaji wa sekta isiyo rasmi nchini. Tathmini hii itafanyika baada ya miaka miwili ya utekelezaji wa mradi na itaangalia viashiria vifuatavyo:-

a) Pato lililoongezeka kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini;
b) Idadi ya wafanyabiashara walionufaika na fedha za mradi;
c) Ajira zilizozalishwa kutokana na mradi;
d) Shughuli za kiuchumi zilizoboreshwa kutokana na mradi;
e) Idadi ya wafanyabiashara ndogondogo walionufaika kwenye taasisi nyingine za fedha;
f) Mikopo iliyotolewa Kisekta kwa idadi na thamani kwa mfano Kilimo, Mifugo, Viwanda n.k;
g) Idadi ya wafanyabiashara ndogondogo waliohitimu na kuwa wafanyabiashara wa kati au wakubwa wanaoingia kwenye mfumo rasmi; na
h) Idadi ya wafanyabiashara ndogondogo waliopata mafunzo ya fedha na elimu ya ujasiriamali.

## 5.2 Utunzaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Utoaji Mikopo

Mfumo wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za Mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini utakuwa kama ifuatavyo:-

i) Taasisi ya Fedha husika itaandaa taarifa ya kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka ya utoaji mikopo na urejeshaji wake kwenye akaunti maalum na kuwasilisha Wizara yenye dhamana na Makundi Maalum kwa hatua zaidi; na

ii) Muda wa kuwasilisha taarifa hiyo utakuwa ndani ya siku 15 ya mwezi unaofuata.

## 5.3 Mapitio ya Mwongozo

Mapitio ya Mwongozo yatafanyika kulingana na mahitaji ya wakati husika. Mapitio hayo yatasaidia kwenye uboreshaji wa huduma za utoaji mikopo hiyo ili uweze kufikia malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

## 5.4 Ukaguzi wa Fedha za Mikopo

i) Ukaguzi wa fedha za mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo utafanyika kwa kuzingatia taratibu za ukaguzi wa hesabu za Serikali; na

ii) Ukaguzi mwingine unaweza ukafanyika itakavyoonekana inafaa kati ya Wizara yenye dhamana na Makundi Maalum na Wizara ya Fedha.

## 5.5 Uwajibikaji Wakati wa Utekelezaji wa Shughuli za Utoaji Mikopo

Mtu yeyote atakayebainika kutumia fedha za mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo kwa ajili ya maslahi yake binafsi au shughuli ambazo hazihusiani na lengo lililokusudiwa atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za nchi.

# SURA YA SITA

# HITIMISHO

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu itakayowezesha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara ndogondogo nchini kupitia Taasisi za Fedha ili kuleta ufanisi uliokusudiwa na Serikali. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wafanyabiashara ndogondogo wanaongeza kipato chao na kufikia hatua ya kuwa wafanyabiashara wa kati na wakubwa wanaochangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Hivyo, ngazi zote za utekelezaji wa Mwongozo huu hazina budi kuhakikisha kuwa walengwa wanapatiwa huduma bora zinazokidhi matarajio ya Serikali.